

TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI WA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA KILIMO WILAYANI (DASIP)

WARSHA YA MAPITIO YA KUBORESHA UTEKELEZAJI WA
MIPANGO YA MAENDELEO YA KILIMO YA WILAYA
(DADPs)

Charles R. Tulahi
Mratibu wa Mradi
DASIP


MWANZA, 05 - 06 SEPTEMBER 2008






MADHUMUNI YA MRADI

Kuongeza tija na pato la mkulima
na mfugaji




- 
- # NAFASI YA MRADI
- ❖ DASIP ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP)
 - ❖ Katika ngazi ya Wilaya DASIP ni sehemu ya DADPs
 - ❖ Katika ngazi ya Kijiji DASIP ni sehemu ya VADPs

ENEOLA MRADI


- **Kigoma:** Kasulu, Kibondo and Kigoma (V);
- **Kagera:** Ngara, Karagwe, Muleba, Chato, Biharamulo, Missenyi na Bukoba (V);
- **Mara:** Bunda, Serengeti, Rorya, Tarime, na Musoma (V);
- **Shinyanga:** Bariadi, Bukombe, Kahama, Kishapu, Maswa, Meatu na Shinyanga (V);
- **Mwanza:** Geita, Kwimba, Magu, Misungwi, Sengerema na Ukerewe.



DADP



VADP



SEHEMU KUU ZA MRADI

1. Kujenga uwezo wa wakulima
2. Kujenga uwezo wa Kuandaa mipango ya Kilimo ya Wilaya na Vijiji na Uwekezaji
3. Kuimarisha huduma za fedha na Masoko
4. Kuratibu Mradi (PCU)



TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI



1. Kujenga uwezo wa Wakulima

Lengo:

- Kuunda vikundi vya wakulima 10,000 (Vikundi zaidi ya 12 kila kijiji cha DASIP)
- Kila Kikundi cha watu 25 (50% wanawake) kuanzisha mradi mdogo baada ya kufuzu mafunzo ya Shamba Darasa
- Wakulima watakao fuzu kuhamishia mbinu walizojifunza kwenye mashamba yao






Kazi zilizofanyika

(i) Kujenga uwezo wa Wataalam

- Wataalam 56 wa wilaya na 685 katika ngazi za Kata na Kijiji wamepata mafunzo ya kuunda vikundi na kutoa mafunzo kwa kutumia mbinu ya Shamba Darasa
- Wataalam 50 ngazi ya wilaya (DTCs) wamepatiwa pikipiki na vitendea kazi vingine





(ii) Kujenga Uwezo wa Wakulima

- Vikundi 1,484 vimepatiwa mafunzo kwa kutumia mbinu ya Shamba Darasa
- Vikundi 1,450 Vimefuzu na kupelekewa fedha kwa ajili ya kuanzisha miradi midogo





TATIZO


- Wakulima hawajawezeshwa kiasi cha kutosha kuelewa uwezo wao na kuutumia/ wamejengewa mazingira ya utegemezi uliojengwa na baadhi ta asasi



Changamoto


- Kuunda na kufundisha Vikundi angalau 6 katika kila kijiji kwa mwaka kuanzia 2008/09
- Kuhamisha ujuzi kutoka Shamba Darasa kwenda kwenye mashamba ya wakulima





- Kuwezesha vikundi vilivyoundwa kuwa endelevu na kupanua shughuli zao
- Kuandaa Mashamba Darasa Kwa Utaratibu utakaowezesha Kuzalisha mazao yenye ubora na **kiasi** kinachokidhi mahitaji ya soko





- Kuweka mpango utakaowezesha wakulima kuzalisha mazao kwa kiasi cha kuwaondolea umaskini (**Mbinu Bora + Eneo** kwa kila mtu kwenye familia)- *Economic Unit of Production*
- Kuwezesha wakulima kutambua fursa na uwezo wao na kuutumia




2. Kujenga uwezo wa Kuandaa mipango na Uwekezaji

LENGO

- Kujenga uwezo wa vijiji 780 wa kuandaa VADPs nzuri
- Kujenga uwezo wa Wilaya 28 wa Kuandaa DADPs
- Kuwezesha vijiji 780 kutekeleza miradi ya Jamii - kila kijiji mradi wa thamani ya sh. Milioni 35 au zaidi (kila kijiji kimetengewa sh. Milioni 28 za DASIP na kinatakiwa kuchangia sh. Milioni 7.0)





- Kuwezesha Wilaya kutekeleza Miradi ya Kati : Km 20 za barabara + miradi ya umwagiliaji (Sh. Milioni 11 kwa kilometa moja na sh. Milioni 225 kwa miradi ya Umwagiliaji kwa Wilaya)
- Kupanua Matumizi ya Teknolojia za kilimo (Shilingi milioni 5 na michango ya jamii sh. Milioni 5 au zaidi)





Kazi zilizofanyika

- Timu 28 za wawezeshaji za Wilaya (DFT) zimepatwa mafunzo ya kuandaa VADPs na DADPs
- Timu 497 za wawezeshaji za Kata (WFT) zimepata mafunzo ya kuandaa VADPs
- DADPs 56 zimeandaliwa





- VADPs 780 zimeandaliwa
- Pikipiki 50 zimenunuliwa na kupelekwa Kwenye halmashauri
- Compyuta na *Phocopiers* zimepelekwa kwenye Halmashauri 25

NB:Halmashauri mpya za Rorya, Missenyi na Chato zipo katika hatua za awali za ununuzi wa pikipiki, compyuta, photocopiers na vifaa vingine





2. Miradi ya jamii

- Miradi 100 ya "*Quick Win*" imetekelezwa. 61 tayari imekamilika
- Miradi 516 tayari imepelekewa fedha, (bilioni 5.478) na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji



Utekelezaji wa Miradi YA JAMII 'Quick Win' Projects 2006/2007




	Mwanza	Shinyanga	Kagera	Mara	Kigoma	Jumla	% ya Jumla
Malambo	4	0	1	1	1	7	11
Vibanio vya Ng'ombe	0	0	6	0	0	6	10
Majosho	6	5	5	7	4	27	44
Mashine ya Kukuoboa	0	0	1	0	0	1	2
Kahawa (Robusta)							
Machinjio	0	0	2	1	0	3	5
Masoko	1	1	0	0	1	4	7
Barabara za Vijijini	0	0	1	0	1	2	3
Umwagiliaji	2	4	0	2	0	7	11
Mashine ya Kukuoboa	0	0	0	1	0	1	2
Kahawa (Arabica)							
Maghala	1	1	0	0	0	2	3
Visima Vifupi	1	0	0	0	0	1	2
JUMLA	15	11	16	12	7	61	100
% ya Jumla Kimkoa	25	18	26	20	11	100	



MIRADI YA JAMII YA MWAKA 2007/08


Na.	Mkoa	Idadi ya Miradi	Gharama (Tsh. '000)		
			Mchango wa Jamii	Mchango wa Mradi	Jumla
1	Mwanza	130	430,890	1,425,023	1,855,913
2	Shinyanga	150	490,186	1,825,900	2,316,086
3	Mara	121	308,154	916,206	1,334,360
4	Kagera	81	197,999	715,121	913,120
5	Kigoma	34	150,635	596,541	747,176
	Jumla	516	1,577,864	5,478,791	7,056,655





MIPADI YA JAMII YA MWAKA 2009/10

Na.	Mkoa	Idadi ya miradi	Gharama (Tshs.'000)		
			Mchango wa Jamii	Mchango wa Mradi	Jumla
1	Kagera	149	695,495	2,879,655	3,575,150
2	Kigoma	26	201,131	845,305	1,046,436
3	Mara	138	573,846	2,085,309	2,659,155
4	Mwanza	124	596,583	2,818,531	3,415,114
5	Shinyanga	128	797,261	3,157,645	3,954,906
Jumla		565	2,864,316	11,786,445	14,650,761



Matatizo

- i. Kuchelewa kwa utekelezaji wa Miradi
Miradi mingi ya jamii haijakamilika au
haijaanza kutekelezwa
- ii. Kupanda kwa gharama za kutekeleza
miradi kutokana na kuchelewa kuanza
utekelezaji, m.f. ununuzi wa baiskeli;
- iii. Kutozingatiwa kwa sheria na kanuni za
ununuzi
- iv. Ushirikiano mdogo katika kuhudumia miradi
ya kilimo kutoka Idara zingine za
Halmashauri





V. Kutenganisha miradi ya DASIP na DADPs: Fedha za *Basket Fund* kutogharamia shughuli ambazo DASIP ina ukomo;


VI. Ubora hafifu wa baadhi ya miradi inayotekelezwa



Changamoto

- Kuandaa VADPs na DADPs shirikishi na Jumuishi,
- Kujenga miradi midogo ya jamii na ya kati na kuikamilisha Katika miaka miwili ijayo (*Micro-projects and Medium scale projects*);
- Kuimarisha uwajibikaji na usimamizi wa miradi ya Jamii






- Kuwezesha jamii kuibua miradi inayotatua matatizo ya msingi ya wakulima na wafugaji;
- Kuimarisha taratibu za ununuzi na fedha na kuhakikisha zinafuatwa



3. Kuimarisha huduma za Fedha na Masoko

- Eneo hili lipo katika hatua za awali za utekelezaji. Wataalamu waelekezi wanatarajiwa kuanza kazi mwezi huu wa Septemba kwa ajili kufanya utafiti wa namna sahihi na bora ya kutoa huduma hizo





Changamoto

1. Kuimarisha na kuboresha huduma za fedha kwa kiwango kitakachowawezesha wakulima kuzitumia na kunufaika nazo;
2. Kujenga mifumo ya masoko itakayowawezesha wakulima na wafugaji kushiriki na kunufaika na mfumo wa soko huru.






Uratibu wa Miradi

- Kitengo cha Kuratibu Miradi (PCU) kimekuwa kikiratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mradi. Kazi ambazo zimefanyika :
- Kutuma fedha kwenye Halmashauri husika na kufuatilia matumizi yake,
- Kutoa miongozo ya utekelezaji wa Mradi, matumizi ya fedha na ununuzi wa bidhaa na huduma,





- Kufuatilia utekelezaji wa Mradi,
- Kuandaa mafunzo na mikutano mabalimbali,
- Kutoa ushauri kuhusu ununuzi, matumizi ya fedha na utekelezaji wa miradi,







MAFANIKIO

1. Wataalam katika ngazi mablimbali wamepata mafunzo na wanajua majukumu wanayopaswa kufanya
2. Wakulima wameanza kujua Mradi na kudai fedha na huduma wanazopaswa kuzipata;
3. Miradi iliyotekelezwa vizuri imepunguza matatizo yaliyokuwa yanaikabili jamii; m.f, majosho, mashine za kuongeza thamani ya mazao, maghala, magulio, malambo n.k .



- 
- 
4. Wakulima na wafugaji wamepata utaalum kupitia Mashamba Darasa.


 6. Kuna Wilaya ambazo viongozi wa wilaya wameonyesha kushiriki kikamilifu katika kusimamia na kufuatilia shughuli za Mradi.

MWELEKEO

1. Kuongeza kasi ya kutekeleza miradi ya Kati na ya Jamii (*medium scale Projects + Micro-projects*)
2. Kuunda vikundi vya wakulima (PFGs) na kufikia vikundi angalau 12 kila kijiji katika miaka miwili ijayo.
3. Kuboresha uandaaji na usimamizi wa DADPs
4. Kuimarisha mfumo wa usimamizi, ufuatiliaji na tathmini.



5. Kuimarisha huduma za Fedha na Masoko - Mchakato wa kuanza kutekeleza eneo hili upo katika hatua za awali. Utekelezaji utazishirikisha Wilaya zote za DASIP.



MWISHO

